

YESU HUJA WA UWEZA

Traditional Harmny
Typed by: Victormwafrika
2022-Mbuyuni Dodoma

$J=100$

1.Ye su hu ja kwa u wezo pe nye pe ndo, ma i sha ye

nye hu zu ni hu cha nga msha, Pe ndo hu tu fu ndi sha,

i pa sa vyo ku mwo mba, Ma jo nzi hu o ndo shwa pe

Chorus...

nye pe ndo; Pe ny'e pe ndo, pe ny'e pe - ndo, mi o yo - hu

i mba nyimbo pe ny'e pe ndo; pe ny'e pe - ndo, ny'e pe - ndo

Fu ra ha A ma ni zi po pe nye pe ndo.

2. Mwanadamu hutulia penye pendo, kazi hufanywa kwa moyo penye pendo,
Watu husameheana, moyo huwa salama, Maisha ni adhimu penye pendo,.....

3. Huzuni huwa furaha penye pendo, mzigo huwa mwepesi penye pendo,
Na upendo ni mwanga, hutuonyesha njia, Heri wale walio penye pendo,.....

4. Umoja na Amani ni penye pendo, Viongozi wa kweli ni penye pendo,
Bwana tujalie pendo, na tushirikiane, kwa Urafiki kweli penye pendo.....